Yesu Ututoni

TRUEWAY KIDS.COM

Utangulizi

Katika somo hili, tutajifunza kuhusu maisha ya Yesu alipokuwa mtoto. Biblia haisemi mengi kuhusu maisha yake kati ya kuzaliwa na huduma yake, lakini tuna kifungu kimoja kinachopatikana katika Luka 2:41-52.

Baadhi ya mambo muhimu tutakayozingatia ni:

- Yesu alifanyika mwanadamu na akakua kama sisi.
- Yesu alilipenda Neno la Mungu na nyumba ya Mungu.
- Lazima tuwe waangalifu tusije tukamsahau Yesu.

Mwongozo wa Somo

Anza somo la wiki hii, kwa kutafakari baadhi ya mambo ambayo tayari tumejifunza. Uliza mtoto wako kama anakumbuka Yesu alizaliwa wapi? Bethlehemu. Shiriki jinsi baada ya kuishi kwa muda huko Misri ili kujificha kutoka kwa Mfalme Herode, Yusufu, Mariamu, na Yesu kurudi Nazareti. Sisitiza jinsi Yesu aliishi maisha ya kawaida kama sisi. Alikuwa akila kifungua kinywa, chakula cha mchana na chakula cha jioni. Shiriki jinsi Mariamu na Yusufu pia walipata watoto wengine. Yesu alikulia katika familia ya kawaida. Eleza jinsi Yesu alihudhuria shule ya sinagogi ili kujifunza kuhusu Agano la Kale.

Soma Luka 2:40. Ongelea jinsi Yesu alivyokua:: 1) Alikua katika hekima. Alijifunza mambo shuleni, katika sinagogi (kanisa), na kutoka kwa wengine. 2) Alikua kimwili. Alikula vizuri na kukaa vizuri ili aweze kukua na kuwa na nguvu. 3) Alikua kiroho.

Alijifunza Biblia, akasali na kumpenda Mungu. 4) Alikua kijamii. Alifanya marafiki na kuwatendea wengine jinsi alivyotaka kutendewa.

Shiriki jinsi tunapaswa pia kukua katika maeneo hayo. Toa mifano ya njia ambazo tunakua katika maeneo hayo. Jaribu kutafuta picha au nguo za zamani za mtoto wako, ili kuwakumbusha jinsi walivyokua kimwili. Wape baadhi ya kazi rahisi za kufanya, kama vile kula peke yao na wakumbushe jinsi ambavyo hawakuweza kufanya hivyo walipokuwa watoto.

Shiriki jinsi Yesu alipokuwa na umri wa miaka 12, alienda pamoja na familia yake huko Yerusalemu kusherehekea Sikukuu ya Pasaka. Kumbuka: Kwa watoto wa shule ya awali, kumi na mbili ni KUBWA. Wanaweza hata kutowafikiria kama mtoto. Jaribu kufikiria mtu unayemjua ambaye ana umri wa miaka 12. Ikiwa uko kanisani, labda unaweza kumwomba mwenye umri wa miaka kumi na mbili kuja katika darasa lako.

Zungumza jinsi sheria ilivyowataka watu kusherehekea Pasaka na karamu zingine. Tafakari juu ya Pasaka na jinsi Mungu alivyowaokoa watu wake kutoka Misri.

Fikiria kuhusu baadhi ya sherehe ambazo tunasherehekea na yale zinatufundisha kuhusu Mungu.

Krismasi, Pasaka, Pentekoste nk.

Shiriki jinsi walipokuwa wakirudi kutoka Yerusalemu, Mariamu na Yosefu walitambua kuwa Yesu hayupo. Unaweza kushiriki hadithi kuhusu kupotea au kuhusu mhusika wa kubuni ambaye alipotea katika duka kubwa. Fikiria juu ya hisia za mtoto na wazazi.

Zungumza kuhusu jinsi ambavyo ni muhimu kila wakati TUWE karibu na wazazi wetu na kushika mikono yao katika sehemu zenye shughuli nyingi na misongamano ili tusipotee.

Fikiria kuhusu nyakati fulani ambapo tunasahau kuhusu Yesu. Labda tunafanya jambo baya, na tukijua kuwa Yesu hangependezwa kwa sababu tunasahau kusali na kufikiria kile kinachompendeza.

Zungumza jinsi Mariamu na Yosefu walivyomtafuta Yesu kila mahali, na wakamkuta hekaluni akiwafundisha walimu. Shiriki kwamba ingawa Alikuwa mdogo, Aliipenda Biblia na alitaka kuizungumzia kwa wengine. Waambie mtoto wako jinsi unavyopenda anaposhiriki nawe yale ambayo amejifunza katika Biblia.

Shiriki jinsi Yesu alirudi nyumbani pamoja na Mariamu na Yosefu. Yesu alijua jinsi ilivyokuwa muhimu kuwatii wazazi wake.

© 2023 truewaykids.com

Mariamu na Yusufu walimwambia Yesu kuwa ni wakati wa kurudi nyumbani.

Yesu alisafiri kurudi Nazareti pamoja na Mariamu na Yusufu.

Alijua ni muhimu kuwatii wazazi wake.

Mariamu alithamini nyakati hizi moyoni mwake. Yesu aliendelea kukua.

Mtoto Yesu atembelea Hekalu

Yesu alipokuwa mtoto, aliishi Nazareti pamoja na familia yake.

Yesu alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili, alisafiri na familia yake hadi Yerusalemu katika sherehe maalum.

Ilichukua siku nyingi kufika huko. Yerusalemu lilikuwa jiji kubwa lenye hekalu kubwa.

Baada ya sherehe, ilifikia wakati wa kusafiri kurudi Nazareti.

Wakiwa njiani kurudi, Mariamu na Yosefu walitambua kuwa Yesu hayupo/haonekani.

Walienda kuangalia kama alikuwa anacheza na binamu yake au rafiki yake, lakini hakuwepo.

Walikuwa na wasiwasi sana na wakarudi Yerusalemu kumtafuta.

Walimkuta Yesu angali bado akiwa hekaluni akijifunza na kuzungumzia juu ya Biblia.

Aliifurahia sana, Alikuwa yupo bado (hekaluni).

Makuhani katika hekalu walistaajabishwa na uelewa wake.

Michezo na Shughuli

CHEZA SHULE

Waambie watoto wako wajifanye wanacheza shule. Unaweza kuandaa darasa la kujifanya (kuigizia) lenye ubao wa kuandikia na shughuli za kufanya. Ruhusu mtoto wako asimamie shughuli hiyo. Sio tu kwamba itakuwa ya kufurahisha mnapokuwa mkijifunza kwa pamoja, lakini pia itaimarisha kujifunza kwao kupitia ufundishaji. Zungumza kuhusu jinsi Yesu alivyojifunza na kufundisha.





VITU VILIVYOPOTEA

Kwa mchezo huu, unaweza kuficha vitu au kutumia vitu ambavyo tayari vipo. Mtu mmoja anajifanya kutoa tangazo. "Mabibi na Mabwana, tumepoteza ...., ikiwa itapatikana, tafadhali irudishe kwa ...." watoto wengine watafute kitu hicho chumbani haraka iwezekanavyo na irudishe mahali au mtu sahihi.

PANDA BAADHI YA MBEGU

Tafuta mbegu ambazo ni rahisi kukuza. Giligilani inakua vizuri wakati wowote wa mwaka. Ongea kuhusu jinsi mbegu inakua, lakini tunahitaji kumwagilia na kuipa mwanga.

Tafakari jinsi Yesu alivyokua kutoka kuwa mtoto mchanga na jinsi Mungu anavyotaka tuwe ndani yake.

© 2023 truewaykids.com

Linganisha mtoto na wanyama wazima

© 2023 truewaykids.com

12

Paka rangi katika mishumaa kumi na miwili



12 12 12 12

Paka rangi miduara yenye namba 12

12 10 16 12

9 12 15 11

© 2023 truewaykids.com

Kila ua limekua kwa urefu gani?



© 2023 truewaykids.com

Wasaidie Mariamu na Yusufu kumpata Yesu hekaluni



© 2023 truewaykids.com

Chati ya Ukuaji

Unachohitaji:

Kiolezo kwenye karatasi nyeupe au kadi

Penseli za kuchorea

Mkasi

Gundi

Nini cha kufanya:

Paka rangi katika sehemu ya mstari wa Biblia. Acha miraba wazi.



Kata kiolezo na ugundishe mahali palipoonyeshwa.

Paka rangi kwenye miraba ili kuendana na urefu wa mtoto. Kila wakati tumia rangi tofauti. Ongeza na tarehe.

© 2023 truewaykids.com

Gundisha hapa

Lakini kuweni

Gundisha hapa

katika neema na

Gundisha hapa

katika kumjua

© 2023 truewaykids.com

Gundisha hapa

bwana wetu na

Gundisha hapa

Mwokozi Yesu

Kristo. 2 Petro 3:18

© 2023 truewaykids.com



© 2023 truewaykids.com

© 2023 truewaykids.com



© 2023 truewaykids.com

Muda wa kuabudu

Agiza kuimba wimbo wa kuabudu. Siyo ulioandaliwa na Trueway Kids.
Video za Yutube zitumike kwa matumizi binafsi tu.

Read Your Bible, Pray Every Day

https://youtu.be/PYRyJxs9CG4

God Is Always Working

https://youtu.be/JiaRAXhGS0U

Obey, Obey The Lord

https://youtu.be/glD4-xl1Amg

Muda wa maombi

Mshukuru Mungu kwa neno lake.

Muombe akusaidie kukua na kuwa zaidi kama Yesu.

Juma lijalo

Yohana Mbatizaji

Kama bado hujafanya hayo, jiunge kwa barua pepe ili kupokea somo la wakati ujao.
truewaykids.com/subscribe/

© 2023 truewaykids.com